

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## BENKI KUU YA TANZANIA



14 Machi 2025

### **TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UFUNGUAJI WA AKAUNTI ZA DIASPORA**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuutarifu umma kwamba taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kwamba Watanzania wanaoishi nchi za nje (Diaspora) wanashindwa kufungua akaunti za benki na kulazimika kufuata kadi zao hapa nchini, hazina ukweli.

Ufutiliaji uliofanywa na Benki Kuu katika benki za hapa nchini umebaini kwamba taratibu zilizopo kwa wateja wa Diaspora ni rafiki na za haraka. Katika kuhakikisha kuwa Diaspora wanapata huduma kwa wakati, benki husika zimefungua madawati mahsusii ya kuwashudumia wateja hao na nyingine zimeanzisha vifurushi maalumu vya Diaspora.

Katika ufunguaji wa akaunti za Diaspora wa Tanzania, mteja anatakiwa kuwa na Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au hati ya kusafiria. Vitambulisho hivyo vinaweza kuwasilishwa kwenye dawati la benki husika au kutumwa kwa njia ya mtandao kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Baada ya Akaunti kufunguliwa, mteja ana uhuru wa kuchukua kadi yake mwenyewe kwa kwenda kwenye benki husika endapo yupo hapa nchini, au kuielekeza benki yake namna anavyotaka kutumiwa kadi hiyo ili imfikie mahali aliko.

Kwa taarifa hii, Diaspora wa Tanzania wanahimizwa kuendelea kutumia benki zetu katika kupata huduma zao na hivyo kuchangia katika maendeleo na uchumi wa taifa letu. Aidha, benki za biashara zinahimizwa kuendelea kutoa elimu kuhusu huduma zao kwa wananchi wote, wakiwemo Diaspora wa Tanzania, ili waweze kujua taratibu zinazotakiwa kufuatwa, nyaraka za msingi, na kupatiwa huduma stahiki kwa wakati bila changamoto zozote.

Benki Kuu inaunga mkono jitihada za Serikali za kuwashimiza Diaspora wa Tanzania kuwekeza nchini kwa ajili yao na maendeleo ya uchumi wa taifa letu; na hivyo itaendelea kufuatilia ili kuhakikisha endapo kuna mteja mwenye changamoto mahsusii kwenye benki yoyote, inatatuliwa na kumuwezesha kupata huduma za kibenki kwa ukamilifu na haraka.

Emmanuel M. Tutuba  
**GAVANA**